

Kijarida cha Mountain View

Septemba 25, 2019

Jumatano, Septemba 25...Mikutano ya Wazazi/Walimu
Alhamisi, Septemba 26.....Mikutano ya Wazazi/Walimu
Ijumaa, Septemba 27.....Hakuna Shule

Ujumbe wa Mwalimu Mkuu

Asante kwa kufanya mipango ya kukutana na walimu wa watoto wako wakati wa mikutano ya wazazi/walimu. Nina uhakika kwamba utapata maelezo muhimu kuhusu mwalimu wako, Mountain View, na mtoto wako. Pia utapata maelezo zaidi kuhusu njia ambazo unaweza kusaidia elimu ya watoto wako. Wanafunzi wanatarajiwa kujifunza nyenzo ngumu zaidi kuliko hapo awali shuleni, na kuna njia nyingi ambazo wewe ukiwa nyumbani na waalimu shuleni mnaweza kushirikiana ili kuwasaidia katika kukabiliana na changamoto hii. Asante kwa kuchukua muda ili kuonyesha watoto wako jinsi walivyo muhimu kwako

Eneo Lipya la Kuacha/Kuchukua

Tuna bahati nzuri kuwa tumepewa eneo jipya kwa wazazi kuacha na kuchukua watoto wao kabla na baada ya shule. Katika barabara, iliyo upande wa Magharibi wa mali ya shule, inatoa fursa ya kutoka California Avenue na kuepuka eneo la maegesho ya gari. Tafadhali hakikisha unaendesha hadi mwisho wa eneo la kuacha unavyoweza kabla ya kuruhusu watoto kuingia ndani na kutoka nje ya gari yako ili tuweze kufanya magari yasafiri bila msongamano na kuhakikisha wanafunzi wapo salama. Tafadhali geuka upande wa kulia unapotoka katika eneo hilo na uingie katika California Avenue. Kujaribu kugeuka kushoto kutafanya msongamano uongezeke zaidi na kuwa hatari. Tunatumai kuwa utatumia eneo letu jipya la kuacha/kuchukua ili kufanya hali yako isiwe ya kuvuruga hisia na kuwa salama zaidi. Asante.

Baraza la Jumuiya ya Shule

Baraza la Jumuiya ya Shule linasaidia kuamua njia bora zaidi ya kutumia bajeti za shule, kuandaa mipango ya maendeleo ya kitaalamu, na kusaidia kujadili na kufanya maamuzi ya kimuundo shuleni mwetu. Baraza hili linakutana mara moja kwa mwezi. Watu wafuatayo wameonyesha nia ya kutumikia kama wanachama wa Baraza la Jumuiya ya Shule: Julianne Rabb, Jennifer Koh, Karla Jimenez, Osman Osman, Daniel Lingsary, Nichole Swink, Elsa Bermudez, Miriam Landeros, Viridiana Cardenas, Jeneanne Lock, Amy Jordan, na Yesica Torres. Mikutano ya Baraza la Jumuiya ya Shule itafanyika katika tarehe zifuatazo katika Kituo cha Mafunzo ya Jumuiya, Chumba cha 185 karibu na jikoni: Oktoba 11, Novemba 8, Disemba 13, Januari 10, Februari 7, Machi 13, Aprili 10, na Mei 8. Mikutano mingine huenda ikaandaliwa kama inahitajika. Mikutano hii huwa wazi kila wakati kwa umma.

Hakuna mfanyakazi wa wilaya au mwanafunzi anayepaswa kubaguliwa kwenye ajira au mpango au shughuli yoyote ya wilaya kwa kigezo cha umri, ulemavu, rangi, jinsi, ujinsi, taarifa za kizazi, uasili wa taifa, ujauzito, kabila, dini, ujinsia, hadhi ya kijeshi. Wilaya imedhamiria kutoa upatikanaji uliosawa na fursa sawa katika mipango yake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, taratibu za malalamiko, upatikanaji wa mpango, matumizi ya mali za wilaya, malazi na masuala mengine ya Fursa Sawa ya Ajira. Wialaya pia inatoa upatikanaji sawa wa mali za wilaya kwaajili ya vikundi vya vijana walioorodheshwa kwenye Sura ya 36 ya Kanuni za Marekani, ikiwemo vikundi vya skauti. Mtu ambaye ametajwa hapa chini ameteuliwa kushughulikia mahitaji na malalamishi yanayohusiana na ubaguzi usiokubalika kisheria, unyanyasaji na na kulipiza kisasi: Tina Hatch, Kufuata sheria na upelelezi, 440 Mashariki 100 Kusini, Jiji la Salt Lake, Utah 84111, (801) 578-8388. Waweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Uraia, Denver, CO, (303) 844-5695.